Keys Educational and Stationery Services (KESS)

# KEYS EDUCATIONAL AND STATIONERY SERVICES (KESS)

## KESS PLATFORM

## NAMBA YA USAJILI: 473801

keyseducationalservices@gmail.com

**0768520832/0658396694**

**KINYEREZI-KIFURU, DAR ES SALAAM**

# MTIHANI WA KWANZA WA UTAMILIFU DARASA LA SABA-2022

# 01: KISWAHILI

**MUDA: SAA 1:40** **ALHAMISI 17, MACHI 2022**

**MAELEKEZO**

- Mtihani huu una jumla ya maswali arobaini na tano (45)
- Jibu maswali yote katika kila sehemu.
- Soma maelekezo yote yaliyoko katika karatasi maalumu ya kujibia (OMR).
- Jaza taarifa zote katika fomu ya OMR na ukurasa wenye swali la 41 hadi 45 katika karatasi ya maswali
- Weka Kivuli katika kila tarakimu ya namba yako ya mtihani kwenye nafasi husika katika fomu ya **OMR**
- Weka kivuli kwenye herufi ya jibu lililo sahihi kwa swali 1 -40.

  Kwa mfano kama jibu ni **A** weka kivuli kama ifuatavyo

  ~~[A]~~ [B] [C] [D] [E]

- Ukigundua kuwa herufi uliyowekea kivuli si jibu sahihi futa kivuli hicho kwa umakini kwa kutumia kifutio safi kabla ya kuweka kivuli katika herufi mpya.
- Tumia penseli ya HB tu katika kujibu swali la 1 hadi 40; na kalamu ya bluu au nyeusi kwa swali la 41 hadi 45
- Simu za mkononi, vikokotozi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

**SEHEMU A (Alama 35)**

Sikiliza kwa makini habari utakayosomewa na msimamizi kisha jibu swali la 1 - 5, **kwa kuweka kivuli katika herufi ya jibu lililo sahihi** katika fomu ya kujibia.

**Maswali**

1. Fikita anapenda sana nini?
   A. Mpira wa miguu  C. Kusoma magazeti  E. Kughani mashairi [ ]
   B. Kusoma hadithi  D. Kuwa fundi seremala
2. Fikita alipewa kiasi gani cha fedha na baba yake?
   A. Shilingi laki moja  C. Shilingi miamoja  E. Shilingi hamsini [ ]
   B. Shilingi miatano  D. Shilingi elfu moja
3. Makala aliyoiona Fikita kwenye gazeti ilikuwa inahusu nini?
   A. Elimu ya Chuo kikuu  C. Afya na Mazingira  E. Malezi bora
   B. Vyuo vya ufundi  D. Kujiajiri [ ]
4. Baada ya kusoma makala kwenye gazeti Ayubu alitamani kuwa nani?
   A. Fundi nguo  C. Fundi seremala  E. Fundi magari [ ]
   B. Fundi umeme  D. Fundi umeme
5. Kwanini Fikita, Ayubu na Temba walipenda masomo ya ufundi?
   A. Kwa sababu walitaka kujiajiri  D. Kwa sababu hawakufaulu kujiunga kidato cha kwanza
   B. Kwa sababu walitaka kuajiriwa  E. Kwa sababu walikuwa wavivu [ ]
   C. Kwa sababu walitaka kuwa mafundi umeme

**Katika swali la 6 - 35, weka kivuli katika herufi ya jibu lililo sahihi katika fomu yako ya kujibia**

6. Wananchi walisimama kidete kupinga nyumba zao kubomolewa ili kupisha upanuzi wa barabara. Kifungu kipi cha maneno kati ya hivi vifuatavyo kinafafanua nahau “kusimama kidete”?
   A. Walipanga nyama  C. Walipinga uamuzi  E. Walikubaliana na uamuzi
   B. Walisimama madhubuti bila woga  D. Waliomba fidia [ ]
7. Nahau ipi kati ya hizi zifuatazo ina maana ya “ kuamua au kutoa uamuzi kuhusu jambo fulani”?
   A. Kujikaza kisabuni  C. Kujifunga kibwebwe  E. Kushika hatamu [ ]
   B. Kula yamini  D. Kukata shauri
8. Baada ya Amani kufika nyumbani alimtoa upepo baba yake. Nahau kutoa upepo kama ilivyotumika katika sentensi hii ina maana gani?
   A. Kumshukuru mtu  C. Kumsaidia mtu  E. Kumkasirisha mtu [ ]
   B. Kumsalimia mtu  D. Kumwomba mtu kitu fulani
9. Mnapenda sana kupiga kelele. Sentensi hii ipo katika nafsi ipi?
   A. Nafsi ya kwanza umoja  C. Nafsi ya pili wingi  E. Nafsi ya tatu wingi
   B. Nafsi ya kwanza wingi  D. Nafsi ya tatu umoja [ ]
10. Mwalimu aliwaambia wanafunzi “yeyote atakayefaulu mtihani huu atazawadiwa”. Sentensi hii ipo katika kauli gani?
    A. Tata  B. Mazoea  C. Taarifa  D. Halisi  E.Jumuishi [ ]
11. Chakula hiki hakiliki maana hakijaiva vizuri. Neno “hakiliki” linaonesha kauli ipi ya utendaji?
    A. Kutenda  B. Kutendwa  C. Kutendeka  D. Kutendea  E. Kutendewa [ ]
12. Mtoto anakula wali kwa kijiko. Katika sentensi hii neno “kwa” limetumika kama aina ipi ya neno?
    A. Kiunganishi  B. Kitenzi  C. Kielezi  D. Kihisishi  E. Kihusishi [ ]
13. Mama aliniambia niweke chakula changu mezani.Ipi kati ya hizi zifuatazo ni kauli halisi ya sentensi hii?
    A. Mama aliniambia kuwa weka chakula chako mezani  D. Mama aliniambia niweke chakula changu mezani
    B. Mama aliniambia “ kiweke chakula chako mezani”  E. Mama alisema “ kiweke chakula changu mezani”
    C. Mama aliniambia “weka chakula changu mezani” [ ]
14. Kamilisha kitendawili hiki: Nimelala ila nachungulia_______
    A. Kaburi  B. Angani  C. Ndotoni  D. Wenzangu  E. Sinema [ ]

15. Methali ipi kati ya hizi zifuatazo ina maana sawa na methali hii " Mchelea mwana kulia, hulia yeye"?
A. Majuto ni mjukuu
D. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
B. Mtaka cha mvunguni sharti ainame
E. Mgaa gaa na upwa hali wali mkavu [ ]
C. Mtaka yote kwa pupa hukosa yote

16. Kifungu kipi cha maneno kati ya hivi vifuatavyo kinakamilisha methali hii: "Bora nusu yai,________"
A. Kuliko yai kamili
C. Kuliko kuku mzima
E. Kuliko ganda tupu [ ]
B. Kuliko kiini cha yai
D. Kuliko yai lenyewe

17. Tunashauriwa kutatua matatizo yakiwa bado madogo kabla hayajaanza kuwa makubwa. Methali ipi kati hizi zifuatazo ina maana sawa na kifungu hicho cha maneno?
A. Hauchi hauchi unakucha
C. Mwanzo wa ngoma ni lele
E. Penye miti hapana wajenzi
B. Usipoziba ufa utajenga ukuta
D. Fimbo ya mnyonge ni umoja [ ]

18. Amini ana mkono mzito. Nahau kuwa na mkono mzito ina maana gani?
A. Kuwa na sifa ya kufanya mambo haraka haraka
D. Kufuata maelekezo unayopewa
B. Kuwa na sifa ya kufanya mambo polepole
E. Kuwa mtu wa kulalamika lalamika [ ]
C. Kuwa mgumu wa kufuata ushauri unaopewa

19. Neno lipi kati ya haya yafuatayo ni jumuishi kwa maneno haya "rukono, simujanja,simutamba,simumtelezo"?
A.Lugha B. Ujumbe C. Mawasiliano D. Masomo E. Simu [ ]

20. Muundo upi unakamilisha sentensi hii "kunywa uji kidogo_______upate nguvu"?
A. Kwa sababu B. Lakini C. Labda D. Walau E. Ingawa [ ]

21. Bwana Pondamali alipofika nyumbani alimkuta mke wake akiwa katika_______la mawazo.
A. Pindi B. Jangaa C. Lindi D. Jungu E. Jimbi [ ]

22. Mwalimu aliwaasa wanafunzi wasome kwa bidii. Nomino ipi inatokana na kubadilishwa kwa kitenzi "asa"?
A. Uasi B. Wosia C. Ushauri D. Onyo E. Asi [ ]

23. Kumbukumbu za mikutano kwa jina lingine huitwaje?
A. Mutahsari B. Riwaya C. Muhtasari D. Rejea E. Ajenda [ ]

24. Neno lipi kati ya maneno yafuatayo **halilandani** na mengine?
A. Ghasia B. Muziki C. Fujo D. Vurumai E. Vurugu [ ]

25. Kipengele kinachoonesha mahali mwandishi alipo katika barua ya kiofisi huitwaje?
A. Anwani ya mwandikiwa
C. Tarehe
E. Anwani ya mwandishi
B. Madhumuni ya barua
D. Saini ya mwandishi [ ]

26. Methali ipi kati ya hizi zifuatazo ina maana sawa na methali isemayo lakuvunda halina ubani?
A. Usione vyaelea vimeundwa
D. Hasira za mkizi furaha ya mvuvi
B. Maji yakimwagika hayazoleki
E. Mgonjwa haulizwi dawa [ ]
C. Nguzo moja haijengi nyumba

27. Kitendawili kisemacho, bibi yuko mlimani anapeta ufuta, kinateguliwa na jibu lipi kati ya haya yafuatayo?
A. Kope B. Macho C. Nyungo D. Kinu E. Mwezi [ ]

28. Mwalimu aliwaamuru wanafunzi wote watoke nje. Neno **nje** lina silabi ngapi?
A. Moja B. Mbili C. Tatu D. Nne E. Tano [ ]

29. Neno linalotokana na kudondosha silabi moja katika neno "dunia" ni lipi kati ya haya yafuatayo?
A. Unia B. Pania C. Duni D. Udi E. Deni [ ]

30. Wananchi wa kijiji cha Kaziramiunda waliafiki wazo la mwenyekiti wao kuhusu kuanzisha shule ya bweni ya wasichana katika kijiji hicho. Kinyume cha neno "waliafiki" kama lilivyotumika katika sentensi hii ni kipi?
A. Walikubali B. Walipinga C. Walishauri D. Waliomba E. Waliruhusu [ ]

31. "Akimchukua hamrudishi". Jibu la kitendawili hiki ni lipi kati ya haya yafuatayo?
A. Usingizi B. Huzuni C. Furaha D. Kifo E. Maji [ ]

32. Nyumba au chumba mnamohifadhiwa machapisho ambayo watu huruhusiwa kuyatumia au kuyaazima kwa muda huitwaje?
A. Maabara B. Makumbusho C. Maktaba D. Mkutubi E. Nyaraka [ ]
33. "Mwalimu na mwanafunzi wanaimba wimbo". Wingi wa sentensi hii ni upi?
A. Mwalimu na wanafunzi wanaimba wimbo
B. Walimu na wanafunzi wanaimba wimbo
C. Mwalimu na mwanafunzi wanaimba nyimbo
D. Walimu na mwanafunzi wanaimba nyimbo
E. Walimu na wanafunzi wanaimba nyimbo [ ]
34. Nimepokea taarifa **muhimu** kutoka kwa Mwalimu Mkuu. Neno lililopigiwa mstari katika sentensi hii limetumika kama aina gani ya neno?
A. Kielezi B. Kiunganishi C.Nomino D. Kivumishi E. Kitenzi [ ]
35. Ufupisho sahihi wa maneno "Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa" ni upi?
A. MKUKUTA B. MEMWA C. MEMKWA D. MPEMKWA E. MEKWA [ ]

## SEHEMU B (Alama 5)

Panga hatua za kufanya ufupisho wa habari zifuatazo katika mtiririko sahihi kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E kwa **kuweka kivuli katika herufi ya jibu lililo sahihi** katika fomu yako ya kujibia.

36. Kusoma habari tena kwa mara ya pili [ ]
37. Kupitia ufupisho wa habari ili kuondoa makosa [ ]
38. Kuandika ufupisho wa habari. [ ]
39. Kusoma habari yote ili kubaini mwanzo muhimu [ ]
40. Kubaini wahusika katika habari [ ]

## SEHEMU C (Alama 10)

## UFAHAMU

**Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu swali 41 - 45 kwa kuandika jibu sahihi katika fomu yako ya kujibia.**

Kiswahili naazimu, sifayo inayokabwa,
Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo kubwa,
Toka kama chemchemu, furika palipozibwa,
Titi la mama ni tamu, jingine halishi hamu.

Toka kama mlizamu,juu kwa wingi furika,
Uoneshe umuhimu, kwa wasio kutamka,
Ndipo waingiwe hamu, mapajani kukuweka,
Titi la mama ni tamu, jingine halishi hamu.
.

**Maswali**

41. Shairi hili lina mishororo mingapi?
42. Kila mshororo katika shairi hili umeundwa na mizani ngapi?
43. Andika kirefu cha neno"sifayo" kama lilivyotumika katika mshororo wa kwanza wa shairi hili.
44. Kina cha mwisho katika ubeti wa kwanza ni kipi?
45. Kanuni gani inaelekeza kwamba vina vya mwisho katika shairi la kimapokeo vifanane?